

**KUMB: PPR/12 - 1/03**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA**  
**JUMATANO, TAREHE 7 MACHI 2012**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 7 Machi 2012**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo.

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa aina zote za mafuta zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 01 Februari 2012. Katika toleo hili, bei ya rejareja kwa mafuta aina zote zimepanda kama ifuatavyo: Petroli imeongezeka kwa Sh 153/lita sawa na asilimia 7.67; Dizeli imeongezeka kwa Sh 119/lita sawa na asilimia 6.01; na Mafuta ya taa yameongezeka kwa Sh 104/lita, sawa na asilimia 5.35. Mabadiliko haya ya bei za mafuta hapa nchini yametokana na mabadiliko ya bei katika soko la dunia na kushuka kidogo kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani. Thamani ya shilingi imeshuka kwa asilimia 0.13 ikilinganishwa na thamani ya shilingi katika toleo lililopita. Bei za jumla kwa kulinganisha matoleo haya mawili zimebadilika kama ifuatavyo: Petroli imeongezeka kwa Sh 152.70/lita sawa na asilimia 7.97; Dizeli imeongezeka kwa Sh 118.77/lita sawa na asilimia 6.24; na Mafuta ya taa yameongezeka kwa Sh 104.49/lita, sawa na asilimia 5.57..
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na *fomula* mpya iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 454 la tarehe 23 Desemba 2011.
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenyewe kiwango cha ubora kisichofaa.

## A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (TZS/LT)	Dizeli (TZS/LT)	Mafuta ya Taa (TZS/LT)
<b>Dar es Salaam</b>	2,144	2,095	2,056
<b>Arusha</b>	2,228	2,179	2,140
Arumeru (Usa West)	2,228	2,179	2,140
Karatu	2,246	2,198	2,158
Monduli	2,233	2,185	2,145
Ngorongoro (Loliondo)	2,284	2,236	2,196
<b>Kibaha</b>	2,148	2,100	2,060
Bagamoyo	2,155	2,106	2,067
Kisarawe	2,151	2,102	2,063
Mkuranga	2,154	2,105	2,066
Rufiji	2,171	2,123	2,083
<b>Dodoma</b>	2,202	2,154	2,114
Kondoa	2,235	2,187	2,147
Kongwa	2,200	2,151	2,112
Mpwapwa	2,204	2,155	2,116
<b>Iringa</b>	2,208	2,159	2,120
Kilolo	2,212	2,164	2,124
Ludewa	2,274	2,225	2,186
Makete	2,267	2,218	2,179
Mufindi (Mafinga)	2,218	2,169	2,129
Njombe	2,236	2,188	2,148
<b>Bukoba</b>	2,359	2,310	2,271
Biharamulo	2,333	2,285	2,245
Chato	2,316	2,267	2,228
Karagwe (Kayanga)	2,375	2,327	2,287
Muleba	2,359	2,310	2,271
Ngara	2,324	2,276	2,236
Misenyi	2,367	2,319	2,279
<b>Kigoma</b>	2,375	2,326	2,287
Kasulu	2,361	2,312	2,273
Kibondo	2,339	2,290	2,251
<b>Moshi</b>	2,217	2,169	2,129
Hai (Bomang'ombe)	2,221	2,172	2,133
Mwanga	2,210	2,162	2,122
Rombo (Mkuu)	2,238	2,190	2,150
Same	2,204	2,155	2,116
Siha (Sanya Juu)	2,224	2,175	2,136

<b>Lindi</b>	2,203	2,154	2,115
Kilwa Masoko	2,178	2,129	2,090
Liwale	2,223	2,175	2,135
Nachingwea	2,232	2,183	2,144
Ruangwa	2,230	2,181	2,142
<b>Babati</b>	2,266	2,217	2,178
Hanang (Katesh)	2,276	2,228	2,188
Kiteto (Kibaya)	2,277	2,228	2,189
Mbulu	2,279	2,230	2,191
Simanjiro (Orkasumet)	2,298	2,249	2,210
<b>Musoma</b>	2,322	2,273	2,234
Bunda	2,313	2,265	2,225
Serengeti (Mugumu)	2,367	2,319	2,279
Tarime	2,333	2,284	2,245
<b>Mbeya</b>	2,251	2,202	2,163
Chunya	2,260	2,212	2,172
Ileje	2,264	2,215	2,176
Kyela	2,266	2,218	2,178
Mbarali (Rujewa)	2,235	2,186	2,147
Mbozi (Vwawa)	2,260	2,211	2,172
Rungwe (Tukuyu)	2,260	2,211	2,172
<b>Morogoro</b>	2,169	2,120	2,081
Mikumi	2,184	2,136	2,096
Kilombero	2,207	2,158	2,118
Mahenge	2,217	2,169	2,129
Kilosa	2,187	2,139	2,099
Mvomero	2,179	2,131	2,091
<b>Mtwara</b>	2,216	2,168	2,128
Masasi	2,242	2,193	2,154
Newala	2,248	2,200	2,160
Tandahimba	2,241	2,193	2,153
<b>Mwanza</b>	2,294	2,245	2,206
Geita	2,334	2,286	2,246
Kwimba	2,330	2,281	2,242
Magu	2,302	2,253	2,214
Misungwi	2,299	2,251	2,211
Sengerema	2,326	2,277	2,238
Ukerewe	2,353	2,304	2,265
<b>Sumbawanga</b>	2,316	2,268	2,228
Mpanda	2,351	2,303	2,263
Nkasi	2,330	2,281	2,242
<b>Songea</b>	2,267	2,218	2,179
Mbinga	2,300	2,252	2,212
Namtumbo	2,296	2,248	2,208
Tunduru	2,326	2,277	2,238

<b>Shinyanga</b>	2,272	2,224	2,184
Kahama	2,286	2,238	2,198
Bukombe	2,298	2,250	2,210
Bariadi	2,314	2,265	2,226
Kishapu	2,300	2,252	2,212
Maswa	2,305	2,257	2,217
Meatu	2,312	2,264	2,224
<b>Singida</b>	2,234	2,186	2,146
Iramba	2,246	2,198	2,158
Manyoni	2,219	2,170	2,131
<b>Tabora</b>	2,298	2,249	2,210
Igunga	2,252	2,203	2,164
Nzega	2,262	2,214	2,174
Sikonge	2,309	2,261	2,221
Urambo	2,311	2,262	2,223
<b>Tanga</b>	2,190	2,141	2,102
Handeni	2,169	2,121	2,081
Kilindi	2,204	2,155	2,116
Korogwe	2,183	2,134	2,095
Lushoto	2,193	2,144	2,105
Mkinga (Maramba)	2,204	2,156	2,116
Muheza	2,190	2,141	2,102
Pangani	2,196	2,148	2,108

## **B: BEI ZA JUMLA**

<b>Bei za Jumla - DSM</b>	<b>Petroli</b>	<b>Dizeli</b>	<b>Mafuta ya Taa</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>2,069.81</b>	<b>2,021.34</b>	<b>1,981.77</b>

**Haruna Masebu**  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**EWURA**